

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3

FASIHI

JULAI/AGOSTI 2012

MUDA: SAA 2½

MUUNGANO WA SHULE ZA UPILI – BUNGOMA

MTIHANI WA KUJITATHMINI {JISET} 2012

Maagizo

- a) Jibu maswali **Manne** pekee
- b) Swali la kwanza ni la Lazima**
- c) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani: Tamthlia, Hadithi fupi, Ushairi na Fasihi simulizi
- d) Usijibu maswali **Mawili** kutoka **Sehemu Moja**
- e) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba maswali yote saba yamo

SEHEMU A: RIWAYA

S. A. Mohamed: Utengano

(ALAMA 20)

1. LAZIMA

“Kumbe bwana wewe mjinga eeh. Yupo mtu asiyejua siasa dunia hii? Wandanganye hao wasiokujua, ^{mimi} nakuja viliyvo.”

- a) Eleza muktadha wa dondo hili (alama 4)
- b) Onyesha inavyodhahirika kuwa hapana asiyejua siasa dunia hii (alama 8)
- c) Thibitisha kuwa mnenaji anamjua mnenewa viliyvo (alama 8)

SEHEMU B: TAMTHLIA

Kithaka wa Mberia: Kifo kisimani

2. “Bahati nasibu inapomteremkia mtu, mara nydingine uhalisia huonekana kama ndoto, mambo huwa hayaeleweki kwa urahisi”

- i) Fafanua muktadha wa dondo hili. (alama 4)
- ii) Onyesha bahati inayorejelewa katika dondo hili. (alama 4)
- iii) Eleza jinsi ambavyo watu wengine katika tamthlia walikosa kuteremkiwa na bahati nasibu (alama 12)

SEHEMU C: HADITHI FUPI

K. W: Wamitila: Mayai waziri wa maradhi na hadilti nydingine

Jibu swali la 3 au la 4

3. ‘Kweli ibilisi wa mtu ni mtu! Thibitisha kauli hii kwa kurejelea hadithi zifuatazo (alama 20)

- i) Tuzo
- ii) Pwaguzi
- iii) Msamaria
- iv) Kachukua hatua nydingine

4 “.....Katika ukurasa huu aliona picha ya mamake.....”

- i) Mbali na picha hii, eleza picha nydingine tano alizoziona. (alama 10)
- ii) Hadithi ‘*Mayai waziri wa maradhi’ inamulika matatizo mbalimbali yanayozikabili nchi nydingi za kiafrika.* Thibitisha kauli hii kwa kufafanua matatizo yoyote matano. (alama 10)

SEHEMU D: USHAIRI

5.

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali
Wangu niliyekupenda, leo nitakufukuza

Kuishi umenishinda, waniletea mayaza
Ola vile nimekonda, jasadi nimepooza
Uwache kuniumiza, ni heri mwana kunenda

Ulikuwa wangu nyonda, huba nikaikoleza
Kukupenda kama tunda, embe lenye uliwaza
Ukajigeuza punda, teke umenicharaza
Uwache kuniumiza, ni heri mwana kunenda

Nimekonda kama ngonda, mwandani wanilemaza
Sautiyo ya kinanda, sitaki kusikiliza
Sikutaki bora kwenda, muhibu wanishangaza
Uwache kuniumiza, ni heri mwana kunenda

Mengi ulionitenda, si madogo yakupuza
Nalikupa kila gwanda, uvae na kupendeza
Ulikula na kuwanda, kadiri ulivyoweza
Uwache kuniumiza, ni heri mwana kunenda.

Kinyume ulipokwenda, nilidhani kuteleza
Na wewe hukujilinda, nyendo mbaya kupunguza
Cha kuvunda kisha vunda, hata ukikifukiza
Uwache kuniumiza, ni heri mwana kunenda

Mja wewe wanishinda, kwa tama wachukiza
Kila kitu unadanda, kingawa cha kuumiza
Huwi ndani ya kibanda, huishi kujitembeza
Uwache kuniumiza, ni heri mwana kunenda

- a) Eleza maana ya mleo wa ubeti wa kwanza (alama 2)
- b) Fafanua umuhimu wa kipokeo cha shairi hili (alama 2)
- c) Eleza sifa za kiarudhi katika ubeti wa **tatu** (alama 4)
- d) Taja methali inayodokezwa katika ubeti wa **tano** wa shairi hili (alama 2)
- e) Eleza maudhui ya ubeti wa **pili** wa shairi hili. (alama 2)
- f) Ni jambo lipi zuri ambalo mshairi atalikosa? (alama 1)
- g) Andika ubeti wa **sita** wa shairi hili katika lugha nathari (alama 4)
- h) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi . (alama 3)

- i) Mayaza
- ii) gwanda
- iii) Kuwanda

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

Jibu swal la 6 au 7

- 6 a) Ni nini maana ya **maigizo** katika fasihi simulizi. (alama 2)
- b) Fafanua aina **mbili** kuu za maigizo (alama 4)
- c) Taja sifa zozote **tano** za maigizo. (alama 10)
- d) Eleza dhima zozote **nne** za maigizo (alama 4)
- 7 a) i) Taja njia zozote **tatu** za ukusanyaji wa data katika fasihi simulizi. (alama 3)
ii) Taja mbinu zozote **tatu** zinazotumiwa kuhifadhi fasihi simulizi huku ukionyesha umuhimu wa kuhifadhi fasihi hii. (alama 7)
- b) Eleza maana ya ushairi kwa mujibu wa fasihi simulizi. (alama 1)
- ii) Ni nini maana ya mashairi yafuatayo. (alama 4)
- i) Mashairi ya kifunga nyama
 - ii) Waadhi
- iii) Eleza sifa za ushairi simulizi (alama 8)